# KATIBA YA KITUO CHA HUDUMA ZA SHERIA ZANZIBAR, 1992

# [ZLSC]

**IFANYE HAKI**

**IWE SHAUKU**

**Marekebisho ya 3 ya 2013**

**KATIBA YA KITUO CHA HUDUMA ZA SHERIA ZANZIBAR, 1992**

Utangulizi

IBARA YA KWANZA: Jina la Kituo

IBARA YA PILI: Makao Makuu ya Kituo

IBARA YA TATU: Hulka ya Kituo

IBARA YA NNE: Hadhi ya Kisheria

IBARA YA TANO: Dira

IBARA YA SITA: Dhima

IBARA YA SABA: Madhumuni

IBARA YA NANE: Muundo na Shughuli

IBARA YA TISA: Wadhamini wa Kituo

IBARA YA KUMI: Kusita kuwa Mdhamini

IBARA YA KUMI NA MOJA: Washirika wa Kituo

IBARA YA KUMI NA MBILI: Kusita kuwa Mshirika wa Kituo

IBARA YA KUMI NA TATU: Kikao cha Wadau

IBARA YA KUMI NA NNE: Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo

IBARA YA KUMI NA TANO: Kamati ya Usimamizi ya Kituo

IBARA YA KUMI NA SITA: Watumishi wa Kituo

IBARA YA KUMI NA SABA: Viwango vya Maadili

IBARA YA KUMI NA NANE: Fedha

IBARA YA KUMI NA TISA: Mali na Madeni

IBARA YA ISHIRINI: Mkaguzi

IBARA YA ISHIRINI NA MOJA: Marekebisho

IBARA YA ISHIRINI NA MBILI: Kuvunjwa kwa Kituo

IBARA YA ISHIRINI NA TATU: Ufafanuzi

# KATIBA YA KITUO CHA HUDUMA ZA SHERIA ZANZIBAR, 1992

## UTANGULIZI

*Tukiwa wenye kutaka kuunda jamii ambayo katiba ndiyo inayotawala, utawala wa sheria unaheshimiwa na haki za binadamu zinatekelezwa; jamii ambayo usawa, haki za kijamii, ustahamilivu na utawala bora ndio kaida yake; sisi, wanasheria na wanaharakati wa haki za binadamu, tumeamua kuunda chama kinachoamini na kupigania misingi hii ambayo tunaiamini kwa dhati kabisa.*

## IBARA YA KWANZA

### Jina la Kituo

Jina la Kituo litakuwa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar ambalo katika katiba hii litakuwa ni Kituo au (ZLSC).

## IBARA YA PILI

### Makao Makuu ya Kituo

Ofisi iliyosajiliwa ya Kituo itakuwepo Zanzibar Mjini. Hata hivyo, Kituo kinaweza kufungua ofisi katika sehemu nyingine za Zanzibar.

## IBARA YA TATU

### Hulka ya Kituo

Kituo kitakuwa si cha kiserikali, kisichopendelea chama chochote cha siasa, cha uanachama wa hiari, kilicho huru na kisichokuwa na madhumuni ya kuingiza faida ambacho madhumuni yake makuu ni kutoa huduma za kisheria, msaada wa kisheria na huduma nyingine za kisheria kwa kundi la wale walio hatarini kuathirika na wasio na uwezo katika jamii ya Zanzibar, kutoa elimu ya kisheria na ya haki za binadamu kwa raia, kusambaza elimu ya sheria na kutoa machapisho kuhusu maeneo yote yanayohusiana na sheria kwa watu wa Zanzibar.

## IBARA YA NNE

### Hadhi ya Kisheria

Kituo ni shirika hai kwa hiyo kitakuwa na haki na uwezo wa kushitaki na kushitakiwa kwa jina lake lenyewe na kumiliki mali inayohamishika na isiyohamishika. Kitakuwa na muhuri wake rasmi na Nembo.

## IBARA YA TANO

### Dira

Haki na wote kuweza kuifikia haki.

## IBARA YA SITA

### Dhima

Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar ni Chama kisichopendelea chama chochote cha siasa, kisichokuwa na nia ya kutengeneza faida kilichojitolea kuinua mwamko wa wananchi, kuendeleza Haki za Binadamu na Utawala Bora.

## IBARA YA SABA

### Madhumuni

(1). Madhumuni ya Kituo yatakuwa yafuatayo:

(a). kutoa huduma za kisheria, msaada wa kisheria na huduma nyengine za kisheria kwa wananchi, na hasa kwa wale walio katika hatari ya kuweza kuathirika na sehemu ya jamii ya watu wasiokuwa na uwezo.

(b). kutoa unasihi wa kisheria na uwakilishi kwa masikini, wanawake, watoto, wazee na watu wenye ulemavu ambao wamo katika kutafuta upatanishi, majadiliano, usuluhishi, mashauriano au kufungua madai mahakamani pale huduma ya mwanasheria inapohitajika.

(c). kuendeleza na kutetea mwenendo wa kuheshimu na kutekeleza haki za binadamu, utawala wa sheria, misingi ya demokrasia na utamaduni wa kuwa na amani na uvumilivu;

(d). kufanya shughuli za uthibitishaji kwa mteja yeyote;

(e). kutayarisha mihtasari ya kisheria kwa wateja;

(f). kuwasilisha na kuthibitisha nyaraka;

(g). kutoa ushauri wa kitaalam wa kisheria kwa wananchi;

(h). kutoa elimu ya sheria na ya haki za binadamu kwa wananchi ili kuinua mwamko wa wananchi kuhusu haki zao za msingi na wajubu wao;

(i). kutoa huduma nyengine yoyote inayoweza kutolewa na Mawakili lakini iliyo ndani ya mipaka ya madhumuni na malengo ya Kituo;

(j). kufanya, kuratibu au kuagiza ufanywe utafiti juu ya masuala ya kisheria, na kutoa ushauri katika maeneo yaliyo ndani ya uwezo wa Kituo;

(k). kukusanya na kusambaza taarifa za kisheria na kutunza nyaraka;

(l). kuandaa, kuhariri, kuchapa, kuchapisha, kutoa, kumiliki na kusambaza vitabu, magazeti, majarida na machapisho mengine ya kisheria, na kuanzisha, kuunda, kuendeleza, kukusanya na kufanya maonyesho yanayohusiana na sheria na haki za binadamu;

(m). kuandaa mikutano, warsha na semina ili kuwawezesha wanazuoni na watu mashuhuri kutoka katika nyanja zote za maisha kukutana, kujadiliana na kutunga sera kuhusu sheria, msaada wa kisheria na haki za binadamu;

(n). kuandaa programu za elimu na za kisayansi kwa madhumuni ya kuwapatia mafunzo watu binafsi na vikundi watakaoainishwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa watu hao kunufaika kutokana na mawasiliano yaliyolenga mambo mahasusi yanayotokana na matokeo ya utafiti; na

(o). Kuzisaidia asasi nyengine na watu binafsi ambazo madhumuni yao ni ya ukarimu kwa namna yalivyo ‘ukarimu’ ukiwa na maana ya vile ulivyoelezwa katika sheria za Zanzibar.

(2). Kituo kitafanya vile vile shughuli nyengine zozote zilizo halali kama itakavyokuwa inafaa katika kuyafikia malengo ya kuwa na mwamko mkubwa wa kisheria, kijamii na wa haki za binadamu na kama itakavyokuwa inafaa katika kuyafikia na kuyaendeleza madhumuni ya Kituo kama yalivyo humu.

## IBARA YA NANE

### Muundo na Shughuli

(1). Kituo kimeandikishwa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya Ardhi (Urithi wa Mfululizo) ya mwaka, 1926 (Sura ya 101 ya Sheria za Zanzibar) na wakati wote kitaheshimu Sheria ya Vyama, 1995 (Sheria Na. 6 ya 1995 ya Zanzibar) na kwa sababu hiyo madaraka yote ya kuandikishwa yatakuwa chini ya Wadhamini Waliosajiliwa wa Kituo.

(2). Wadhamini Waliosajiliwa watatumia madaraka yao na kufanya shughuli zao kama itakavyoelezwa katika Kanuni ya Ardhi (Urithi wa Mfululizo) ya 1926 iliyoelezwa na Sheria ya Vyama ya 1995 au sheria husika nyengine yoyote inayotumika.

## IBARA YA TISA

### Wadhamini wa Kituo

(1). Watakuwepo Wadhamini wa Kituo ambao idadi yao, kwa wakati wowote ule haitazidi watano na haitapungua chini ya watatu. Wadhamini wa Kituo ndio watakaokuwa Bodi ya Wadhamini (ambao humu itaitwa Bodi).

(2). Kipindi cha kuwa madarakani cha wajumbe wa Bodi ya Wadhamini kitakuwa ni miaka mitano, kipindi ambacho kinaweza kuongezwa.

(3). Kwa muundo wa Bodi ya Wadhamini, Kituo kitatilia maanani suala la uiano wa kijinsia.

(4). Wadhamini watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wao; ilimradi tu mtu huyo awe na shahada ya kwanza kutoka katika chuo kikuu kinachotambulika.

(5). Wajumbe wa Bodi, **kwa uamuzi wa kauli moja**, wanaweza **kumwalika kwa maandishi**, **mtu mashuhuri mwenye tabia nzuri**, **muadilifu** na **uwezo wa kitaaluma uliothibitishwa**, kujaza nafasi yoyote ile katika Bodi ya Kituo, na ambaye, baada ya kukubali kwake kwa maandishi, atakuwa mjumbe wa Bodi.

(6). Bodi ya Wadhamini itakuwa ndiyo chombo cha kutunga sera cha Kituo.

(7). Bodi itapewa madaraka ya kuhakikisha kuwa Kituo kinaendeshwa kwa ufanisi, kwa namna ya kuleta matokeo na kwa utaratibu mzuri na kinatekeleza madhumuni, sera na maamuzi yake.

(8). Bodi itakutana kwa uchache mara moja baada ya kila miezi mitatu. Unaweza kuitishwa mkutano wa Bodi wa dharura kwa maombi ya Mwenyekiti, Mkurugenzi Mtendaji au wadhamini wawili wowote wale.

(9). Bodi inaweza kuendesha shughuli za kikao katika mkutano wowote ulioitishwa ikiwa kwa uchache angalau wajumbe watatu wamehudhuria.

(10). Miongoni mwa shughuli nyingine ambazo Bodi imepewa na Katiba hii, itasimamia pia utekelezaji wa Viwango vya Maadili vya Kituo na kutekeleza Madhumuni ya Kituo.

(11). Mara kwa mara, na pale inapolazimu, Bodi inaweza kuunda kamati ili kushughulikia masuala mahasusi kwa niaba ya Bodi na kamati hiyo kutoa taarifa kwenye Bodi.

(12). Taratibu za Bodi na za kamati yoyote itakayoundwa na Bodi zitakuwa kama zitakavyoagizwa na Bodi.

(13). Pale ambapo utahitajika ushauri wa kitaalam, Bodi itakuwa na uhuru wa kuwaalika wataalam ili kutoa huduma za ushauri wa kitaalam kwa Bodi.

(14). Shughuli nyingine za Bodi ya Wadhamini zitakuwa:

(a). Kusimamia maendeleo na ustawi wa Kituo;

(b). Kuwa mtunzaji pekee wa rasilimali na maslahi mengine ya Kituo;

(c). Kuandaa Kanuni kwa ajili ya uendeshaji mzuri wa shughuli za Kituo; na

(d). Kushughulikuia mambo yote ya Kituo yanayohusiana na kuvunjwa kwake kwa mujibu wa masharti husika ya Katiba hii.

(15). Wadhamini Waliosajiliwa watatekeleza wajibu wao kwa hiari isipokuwa kama yatakuwepo matumizi au gharama walizozigharamia wao kwa ajili ya au kwa maslahi ya Kituo, basi gharama hizo zitarudishwa.

(16). Wadhamini watakaoajiriwa na au kupitia kwa Kituo kwa ajili ya kazi maalumu ya kitaalam au ushauri watalipwa ipasavyo lakini watatakiwa kutoa asilimia 20% ya malipo hayo kwa Kituo.

(17). Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo atakuwa *mjumbe asiye rasmi* wa Bodi ya Wadhamini na Katibu wa Bodi hiyo.

## IBARA YA KUMI

### Kusita kuwa Mdhamini

(1). Mtu atasita kuwa Mdhamini wa Kituo kwa hali zifuatazo:

(a). Kwa kukubali nafasi ya uongozi katika chama cha siasa, kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, au kuteuliwa kuwa Waziri au Naibu Waziri au uteuzi mwingine wowote wa kisiasa;

(b). Kwa maombi yake yeye mwenyewe kwa maandishi, na maombi hayo kujadiliwa na kukubaliwa na mkutano wa Bodi ya Wadhamini;

(c). Kutohudhuria mikutano mitatu mfululizo ya Bodi bila ya sababu za kimsingi;

(d). Kuwa na tabia ya kufanya mambo ambayo yanakwenda kinyume na maslahi ya Kituo;

(e) Kwa kutokea jambo lolote lile litakaloufanya uanachama wake kuwa mjumbe kukinzana na malengo na madhumuni ya Kituo;

(f). Kutokuwa na uwezo kwa kudumu kulikosababishwa na afya mbaya au sababu nyengine yoyote ile;

(g). Kuzuiliwa kwa mujibu wa sheria yoyote inayotumika; na

(h). kwa kufa.

(2). Wajumbe wa Bodi walio wengi wanaweza, kama wakiona ni lazima, kumwomba mjumbe ambaye anakiuka Katiba ya Kituo, kujiondoa katika nafasi yake. Pindi ombi kama hilo likitolewa, itabidi liheshimiwe.

## IBARA YA KUMI NA MOJA

### Wanachama wa Kituo Walioshirikishwa

(1). Mjumbe yeyote wa Bodi anaweza kumteua mtu maalum aliyejitolea katika kupigania utawala wa sheria, utawala bora na kuheshimu haki za binadamu ili kuwa mwanachama aliyeshirikishwa wa Kituo, ambaye baada ya kukubaliwa na Wajumbe wote wa Bodi, atakuwa Mwanachama aliyeshirikishwa wa Kituo (ambaye katika katiba hii ataitwa Mshirikishwaji).

(2). Mshirikishwaji atakuwa na wajibu wa kuheshimu Katiba hii na Kanuni na Taratibu za Kituo.

(3). Mshirikishwaji lazima awe mtu mwenye uwezo wa kuchukua hadhari kabla ya athari katika kuendeleza sura, hadhi na kazi ya Kituo.

(4). Mshirikishwaji atakuwa na haki ya kujieleza kwa uhuru kabisa juu ya mambo yote yanayohusiana na Kituo.

(5). Mshirikishwaji wa Kituo atakuwa na, miongoni mwa vitu vingine, haki na wajibu ufuatao:

(a). kushiriki kikamilifu katika shughuli za hadhara za Kituo;

(b). Kutumia vifaa vya Kituo;

(c). kunufaika na huduma zote zinazotolewa na Kituo;

(d). kupata habari kuhusu mambo ya Kituo;

(e). kupata machapisho ya Kituo;

(f). kuchukua majukumu na kutekeleza wajibu kama atakavyotakiwa na Bodi ya Wadhamini ya Kituo, Mwenyekiti au Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo; na

(g). kuheshimu masharti ya Katiba hii ambayo itakuwa ndiyo mwongozo mkuu kwa shughuli za Kituo; Kanuni na Taratibu na maagizo mengine ya Kituo.

## IBARA YA KUMI NA MBILI

### Kusita kuwa Mwanachama Mshirikishwaji

(1). Mtu atasita kuwa mwanachama Mshirikishwaji wa Kituo katika hali zifuatazo:

(a). Kufuatia ombi lake mwenyewe kwa maandishi;

(b). Ikiwa mtu huyo, kwa sababu yoyote ile atasita kuendelea kushiriki katika shughuli za Kituo na/au atasita kuchangia katika kuendeleza malengo na madhumuni ya Kituo;

(c). Kwa kutokea jambo lolote lile ambalo litaufanya uanachama wake kukinzana na malengo na madhumuni ya Kituo; au

(d) Kwa kifo chake;

(2). Hatima ya mwanachama Mshirikishwaji kuhusiana na hali yoyote iliyoelezwa katika Ibara ya 11 (1) itajadiliwa na kuamuliwa na Bodi ya Kituo.

## IBARA YA KUMI NA TATU

### Kikao cha Wadau

(1). Patakuwepo na Kikao cha Wadau wa Kituo (katika Katiba hii kitaitwa Kikao).

(2). Kikao cha Wadau kitakuwa na wanachama wasiozidi ishirini na tano watakaoteuliwa na Bodi ya Kituo kwa mapendekezo ya Mkurugenzi Mtendaji kila mwaka kutoka katika jumuiya za kiraia na idara za serikali zinazoshirikiana au kufanyakazi kwa karibu na Kituo au zinazoendesha programu na Kituo.

(3). Madhumuni ya Kikao yatakuwa:

(a). kujadili na kushauri au kupendekeza kwa Bodi ya Kituo mipango, programu na jambo jingine lolote linalokihusu Kituo ambalo limewasilishwa kwenye kikao hicho na Bodi ya Kituo;

(b). Kuanzisha majadiliano juu ya jambo lolote mwafaka kwa Dhima, Dira na Madhumuni ya Kituo kwa madhumuni ya kuboresha kazi ya Kituo;

(c). kusaidia katika kuendeleza na kuimarisha uhusiano kati ya Kituo na Serikali, jumuiya za kiraia na wananchi kwa jumla; na

(d). kupendekeza kwa Bodi ya Wadhamini ya Kituo na Uongozi wa Kituo juu ya utendaji mzuri wa kiueledi, kuimarisha kaida za demokrasia ndani ya Kituo na kudumisha viwango vya hali ya juu vya maadili.

(4). Kikao cha Wadau kitachagua Mwenyekiti wake miongoni mwa wajumbe wake.

(5). Wajumbe wa Bodi ya Kituo watahudhuria mikutano ya Kikao hicho wakiwa wajumbe *wasio rasmi*.

(6). Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo ataiwezesha mikutano ya Kikao hicho.

(7). Kumbukumbu, mapendekezo na ushauri wa kikao vitawasilishwa kwenye Bodi ya Kituo na Mkurugenzi Mtendaji kwa maandishi.

(8). Kikao kitafanyika mara moja kwa mwaka kikiwa kikao chake cha kawaida. Hata hivyo, Wadau wanaweza kuitisha mkutano usio wa kawaida kwa maombi ya, kwa uchache thuluthi moja ya wanachama kwa kushauriana na Mkurugenzi Mtendaji.

## IBARA YA KUMI NA NNE

### Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo

(1). Atakuwepo Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo atakayekuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Kituo.

(2). Mkurugenzi Mtendaji lazima awe na digiri ya sheria kutoka katika chuo kikuu kinachotambulika.

(3). Mkurugenzi Mtendaji atateuliwa na Bodi ya Kituo kwa mapendekezo ya jopo la watu waadilifu wa hali ya juu walioteuliwa na Bodi ili kuteua na kuhoji watu kufuatana na masharti na makubaliano kama yatakavyoonekana yanafaa na Bodi ya Kituo.

(4). Mkurugenzi Mtendaji atakuwa ndiye Afisa Mkuu na Afisa Masuuli wa Kituo na atakuwa na kazi zifuatazo:

(a). kutekeleza maamuzi yote ya kisera yatakayofanywa na Bodi ya Kituo;

(b). Kuchukua hatua kufuatana na utashi wake mwenyewe wa kuendeleza uwezo wa Kituo;

(c). kushughulikia mambo yote yanayohusiana na utawala kwa jumla na fedha za Kituo;

(d). kufanya shughuli za kila siku za kuendesha Kituo; na

(e) kushughulikia nidhamu ya watumishi.

(5). Mkurugenzi Mtendaji atafanya au atasababisha kufanywa kazi zifuatazo:

(a). kuandika na kuweka kumbukumbu za mikutano ya Bodi ya Kituo;

(b). kuhakikisha kuwa kumbukumbu za Kituo zinawekwa vizuri katika ofisi ya Kituo;

(c). kuhakikisha kuwa mali za Kituo zinawekwa na kutunzwa vizuri;

(d). kusimamia uendeshaji mzuri wa shughuli na programu za Kituo;

(e). kutayarisha na kuwasilisha kwenye Bodi ya Kituo, baada ya kila miezi mitatu, ripoti ya shughuli za Kituo na hali ya kifedha ya Kituo;

(f). Kutayarisha taarifa ya mwaka na taarifa ya fedha kwa ajili ya ukaguzi;

(g). kuwa Katibu wa Bodi;

(h). kufanya shughuli nyengine zozote atakazopewa na Bodi ya Kituo au kwa niaba ya Bodi hiyo.

(6). Katika kufanya kazi zake, Mkurugenzi Mtendaji atawajibika kwa Bodi ya Wadhamini ya Kituo itakayokuwa ndiyo yenye mamlaka ya nidhamu kwa ofisi hii.

## IBARA YA KUMI NA TANO

### Kamati ya Usimamizi ya Kituo

(1). Patakuwa na Kamati ya Usimamizi ya Kituo (humu itaitwa Kamati).

(2). Kamati itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a). Mkurugenzi Mtendaji atakayekuwa Mwenyekiti;

(b). Afisa wa Fedha na Utawala atakayekuwa Mjumbe; na

(c). Afisa wa Fedha/Mhasibu atakayekuwa Mjumbe;

(d). Waratibu wa ofisi ndogo za Kituo; na

(e). Mtumishi mmoja atakayewakilisha watumishi atakayeteuliwa/atakayechaguliwa na watumishi.

(3). Shughuli kubwa za Kamati hii zitakuwa:

(a) kufuatilia na kutekeleza maamuzi ya Bodi;

(b). kupitia utendaji wa kazi wa watumishi wa Kituo;

(c). kutathmini maendeleo ya programu za Kituo;

(d). kutoa mapendekezo mbalimbali kwa Bodi; na

(e). kufanya shughuli nyengine yoyote kama itavyoelekezwa na Bodi.

(4). Kamati itakutana kwa uchache mara moja baada ya kila miezi mitatu.

## IBARA YA KUMI NA SITA

### Watumishi wa Kituo

(1). Watakuwepo watumishi wa kituo wa makundi mbalimbali watakaoteuliwa na Bodi ya Kituo kwa makubaliano na masharti ambayo Bodi itayaona yanafaa kwa mujibu wa sheria.

(2). Watumishi wote wa Kituo, isipokuwa Mkurugenzi Mtendaji watawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji.

(3). Watakuwepo watumishi wa kujitolea katika Kituo ambao watachangia katika kazi za Kituo.

(4). Watumishi wa kujitolea wataruhusiwa kufanyakazi katika Kituo na Bodi kwa mapendekezo ya Mkurugenzi Mtendaji na watawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji kwa shughuli zao za kila siku.

(5). Watumishi wa kujitolea watakaotoka nje ya Zanzibar watakuwa na dhama ya kujikimu wao wenyewe na kwa masuala yanayohusu kuishi kwao Zanzibar ikiwa ni pamoja na nyumba na uhamiaji na mahitaji mengine ya kiserikali. Kituo, kwa kuombwa, kinaweza kusaidia katika kuwatambulisha watumishi wa kujitolea serikalini pale patakapokuwepo na vikwazo.

(6). Kwa mchango wao katika Kituo, watumishi wa kujitolea watarudishiwa na Kituo gharama na matumizi waliyofanya kwa ajili ya au kwa maslahi ya Kituo.

(7). Wakati watumishi wakujitolea binafsi wanakaribishwa katika Kituo, umuhimu na kipaumbele vitatolewa kwa watumishi wa kujitolea kutoka au waliopendekezwa na asasi, za hapa nchini na za nje, ambazo zinafanya kazi kwa karibu na kushirikiana na kituo katika nyanja mbalimbali.

(8). Kutakuwepo na makundi mengine ya watumishi wa muda watakaoteuliwa kwa ajili ya miradi na programu mahasusi za Kituo.

(9). Watumishi na watumishi wa kujitolea wa Kituo ambao watakodiwa na au kwa kupitia kwenye Kituo kwa ajili ya kazi maalumu ya kitaalam au ushauri watalipwa ipasavyo lakini watatakiwa kutoa asilimia 20% ya malipo hayo kwa Kituo.

(10). Watumishi wote wa Kituo walio katika makundi mbalimbali watalazimika kutii Viwango vya Maadili vya Kituo.

## IBARA YA KUMI NA SABA

### Viwango vya Maadili

(1). Watu wote wanaoshiriki katika shughuli za Kituo watafanya shughuli zao kwa mujibu wa Katiba hii. Zaidi ya hilo, kila mtu atatarajiwa:

(a). Kuonyesha imani kubwa na ustahamilivu kwa wengine kwa mambo yote yanayohusiana na Kituo.

(b). Kuonyesha tabia ya kuridhisha, uaminifu na uwazi na moyo wa kujitolea kwa shughuli za Kituo;

(c). Kutotumia vifaa vya Kituo, jina au itibari kwa kujipatia maslahi binafsi au maslahi yoyote ya chama cha siasa, kidini, kikabila au maslahi mengine kama hayo ambayo yanakinzana na madhumuni ya Kituo;

(d). Kutokuwa na tabia ambayo inakinzana na maslahi ya Kituo.

(2). Utakuwa ni wajibu wa Bodi ya Kituo kuhakikisha kuwa viwango vya maadili vya Kituo vinaendelezwa.

## IBARA YA KUMI NA NANE

### Fedha

(1). Fedha za Kituo zitapatikana kutokana na vyanzo vile tu ambavyo masharti yake hayatazuia kwa namna yoyote ile utekelezaji wa madhumuni ya Kituo kama yalivyo katika Ibara ya Saba ya Katiba hii au yanayoweza kuyumbisha msimamo na heshima ya Kituo;

(2). Mapato na mali ya kituo, popote itakapopatikana, vitatumika kwa ajili ya kuendeleza madhumuni ya Kituo tu kama ilivyoelezwa katika Ibara ya Saba ya Katiba hii;

(3). Fedha zote zitatumika kwa namna itakavyoidhinishwa na Bodi ya Kituo;

(4). Fedha zote za Kituo zitawekwa katika Benki iliyoidhinishwa na Bodi ya Kituo;

(5). Watakuwepo watia saini wawili kwa hundi za akaunti ya Kituo, ambao ni Muhasibu au Mkurugenzi Mtendaji kwa upande mmoja, na Mwenyekiti na mjumbe mwengine wa Bodi ya Wadhamini, kwa upande mwengine.

(6). Miamala yote itakayofanyika na Kituo au kwa niaba ya Kituo itakuwa kwa jina la Kituo;

(7). Vitabu vya mahesabu vitawekwa makao makuu ya Kituo na hesabu zote za fedha, mezania na ripoti zilizokaguliwa zitawasilishwa kwenye Bodi ya Kituo kila mwaka;

(8). Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo atakuwa ndiye Afisa masuuli wa Kituo.

(9). Mwaka wa fedha wa Kituo utakuwa ni miezi kumi na mbili, kuanzia tarehe 1 Januari na kumalizika tarehe 31 Desemba kila mwaka.

## IBARA YA KUMI NA TISA

### Mali na Madeni

Mali na madeni ya Kituo vitakabidhiwa na kusimamiwa na Wadhamini Waliosajiliwa wa Kituo.

## IBARA YA KUMI NA MBILI

### Mkaguzi

(1). Atakuwepo Mkaguzi wa Kituo atakayeteuliwa na Bodi atakaekuwa na kazi ya kukagua mahesabu yote ya Kituo na kufanya shughuli zote kama inavyotakiwa na sheria iliyopo.

(2). Hakuna Mdhamini, Mjumbe wa Bodi, Mshirikishwaji, Mtumishi au Mfanyakazi wa Kujitolea wa Kituo au jamaa zao au watu wanaowahusu atakayeruhusiwa kuwa Mkaguzi wa Kituo.

(3). Mkaguzi atawasilisha mahesabu yaliyokaguliwa ya Kituo kwa Bodi.

## IBARA YA ISHIRINI NA MOJA

### Marekebisho

Mjumbe yeyote wa Bodi au Mshirikishwaji wa Kituo au mtumishi anaweza kupendekeza marekebisho yoyote yale ya Katiba hii kwa Mwenyekiti wa Bodi au kwa Mkurugenzi Mtendaji, na mapendekezo hayo yatawasilishwa kwa majadiliano na Bodi ya Kituo na azimio lolote kuhusiana na mapendekezo hayo litaamuliwa kwa kukubaliana kwa kauli moja.

## IBARA YA ISHIRINI NA MBILI

### Kuvunjwa

(1). Kituo hakitavunjwa isipokuwa kwa azimio linaloungwa mkono na wajumbe wanne kati ya wajumbe watano wa Wadhamini Waliosajiliwa wa Kituo katika mkutano ulioitishwa mahasusi kwa madhumuni hayo.

(2). Uamuzi wa kukivunja kituo ukishachukuliwa, na baada ya madeni yote kulipwa, mali au rasilimali yote ya Kituo itatolewa sadaka kwa vyama ambavyo madhumuni yao na mwenendo wao, kwa mujibu wa maoni ya Wadhamini Waliosajiliwa, yanakubaliana na madhumuni ya Kituo kama yalivyo katika Ibara ya Saba ya Katiba hii.

## IBARA YA ISHIRINI NA TATU

### Ufafanuzi

(1). Katika katiba hii, isipokuwa kama muktadha unakusudia vingine:

“Mshirikishwaji” ina maana ya mwanachama mshirikishwaji wa Kituo kama ilivyoelezwa na kufafanuliwa na Ibara ya 11 ya Katiba hii.

“Bodi ” ina maana ya Bodi ya Wadhamini ya Kituo kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 9 ya Katiba hii.

“Kituo” ina maana ya kituo cha Huduma za Sheria kama kilivyoelezwa katika Ibara ya 1 ya Katiba hii.

“Mwenyekiti” ina maana ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Kituo kama anavyoteuliwa chini ya masharti ya Ibara ya 9 (3) ya Katiba hii.

“Katiba” ina maana ya Katiba hii inayoanzisha Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar ya 1992 kama itakavyofanyiwa merekebisho mara kwa mara.

“Mkurugenzi Mtendaji” ina maana ya Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo anayeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 14 ya katiba hii.

“Kamati ya Usimamizi” ina maana ya Kamati ya Kituo iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 15 ya Katiba hii.

“Mtumishi” ina maana ya mtu yeyote aliyeajiriwa na Kituo kwa mujibu wa Ibara ya 16 ya Katiba hii.

"Mdau" ina maana ya asasi au idara ya serikali iliyoteuliwa kuwa mdau wa Kituo chini ya Ibara ya 13 ya Katiba hii.

"Muhuri" ina maana ya muhuri wa kawaida wa Kituo kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 4 ya Katiba hii.

"Wadhamini" ina maana ya Wadhamini Waliosajiliwa wa Kituo ambao kuteuliwa kwao na shughuli zao vinaelezwa katika Ibara ya 9 ya Katiba hii.

"Mfanyakazi wa kujitolea" ina maana ya mtu binafsi ambaye si mtumishi wa Kituo lakini anafanyakazi katika au chini ya usimamizi wa Kituo kwa njia ya kujitolea kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 16 ya Katiba hii.

(2). Pale utakapotokea mgogoro wowote kuhusiana na ufafanuzi wa jambo lolote katika Katiba hii, Bodi ya Wadhamini ya Kituo itakuwa na madaraka ya kuusuluhisha mgogoro huo.

IMETHIBITISHWA Zanzibar tarehe 1 Februari, 1992 na kuanza kutumika tarehe 29 Mei 1992.

Marekebisho ya 1 ya Katiba yalifanyika tarehe 8 April, 2001, na kuanza kutumika tarehe 1 Mei, 2001.

Marekebisho ya 2 ya Katiba yalifanyika tarehe 28 Desemba, 2009 na kuanza kutumika tarehe 1 Januari, 2010.

Marekebisho ya 3 ya Katiba yalifanyika tarehe 29 Desemba, 2013 na kuanza kutumika tarehe 1 Januari, 2014.